TAARIFA YA MAELEZO YA CHANJO

# Chanjo ya Tdap

## *Unachohitaji Kujua*

(Pepopunda, Dondakoo na Kifaduro)

Many Vaccine information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis
Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

## 1 Kwa nini nipokee chanjo?

**Pepopunda, dondakoo** na **kifaduro** ni magonjwa hatari sana. Chanjo ya Tdap inaweza kutulianda kutokana na magonjwa haya. Na, wanawake wajawazito wanapopewa chanjo ya Tdap inaweza kuwalinda watoto walio tumboni kutokana na kifaduro.

**PEPOPUNDA** (Pepo punda) ni nadra sana nchini Marekani siku hizi. Ni ugonjwa unaosababisha mkazo na upindani mkali wa misuli, kwa kawaida mwilini mzima.

- Unaweza kusababisha upindani wa misuli katika kichwa na misuli ili usiweze kufungua mdomo wako, kumeza, au wakati mwingine hata kupumua. Pepopunda huua takriban mtu 1 kati ya watu 10 wanaoambukizwa hata baada ya kupokea matibabu bora.

**Dondakoo** pia ni nadra sana nchini Marekani siku hizi. Ni ugonjwa unaosababisha gaga nene kutokea katika nyuma mwa koo.

- Unaweza kusababisha matatizo ya kupumua, kusita kwa moyo, kupooza, na kifo.

**KIFADURO** (Kifaduro) husbabisha kikohozi kikali cha muda mrefu, kinachoweza kusababisha ugumu wa kupumua, kutapika, na kukosa usingizi.

- Pia unaweza kusababisha kupoteza uzani wa mwili, udhaifu, na kuvunjika mbavu. Hadi vijana 2 kati ya 100 na watu 5 wazima katika ya 100 wenye kifaduro hulazwa hospitalini au wana matatizo, yanayoweza kujumuisha nimonia au kifo.

Magonjwa haya husababishwa na bakteria. Dondakoo na kifaduro husambazwa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kupitia unyevu wa kukohoa na kuchichimua. Pepopunda huingia mwilini kupitia mikato, mikwaruzi, au vidonda.

Kabla ya chanjo kugunduliwa, zaidi ya visa 200,000 vya dondakoo, visa 200,000 vya kifaduro, na mamia ya visa vya pepopunda, viliripotiwa Marekani kila mwaka. Tangu chanjo kuanza kupeanwa, ripoti za kesi za pepopunda na dondakoo zimepungua kwa takriban 99% na za kifaduro kwa 80%.

## 2 Chanjo ya Tdap

Chanjo ya Tdap inaweza kuwalinda vijana na watu wazima kutokana na pepopunda, dondakoo, na kifaduro. Dozi moja ya Tdap hupewa mtu mara kwa mara akiwa na umri wa miaka 11 au 12. Watu ambao *hawakupokea* Tdap katika umri huo wanafaa kupokea chanjo hiyo haraka iwezekanavyo.

Tdap ni muhimu hasaa kwa wataalamu wa afya na mtu yoyote anayeingiliana na mtoto mchanga mwenye umri chini ya miezi 12.

Wanawake wajawazito wanafaa kupokea dozi ya Tdao wakati wa **kila ujauzito**, ili kulinda watoto walio tumboni kutokana na kifaduro. Watoto wachanga ndiyo walio katika hatari kubwa ya matatizo hatari ya kutishia maisha ya kifaduro.

Chanjo nyingine, inayoitwa Td, hulinda watu kutokana na peopunda na dondakoo, lakini sio kifaduro. Nyongeza ya Td inafaa kupeanwa kila miaka 10. Tdap inaweza kupeanwa kama moja ya nyongeza hizi ikiwa hujawahi kupokea Tdap hapo awali. Tdap pia inaweza kupeanwa baada ya mkato au kichomo kikali ili kuzuia maambukizo ya pepopunda.

Daktari wako au mtu anayekupatia chanjo hii anaweza kukupatia maelezo zaidi.

Tdap inaweza kupeanwa kwa usalama wakati wowote kama chanjo zingine.

## 3 Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii

- Mtu yoyote ambaye ashawahi kuwa na mzio wa kuhatarisha maisha baada ya kupokea dozi yoyote ya chanjo yenye dondakoo, pepopunda au kifaduro, AU ana mzio mkali dhidi ya sehemu ya chanjo hii, hafai kupokea chanjo ya Tdap. Mwambie mtu anayetoa chanjo kuhusa mizio yoyote hatari.
- Mtu yoyote ambaye ashawahi kuwa katika usingizi mzito au kifafa cha mara kwa mara ndani ya siku 7 baada ya dozi ya utotoni ya DTP au DTaP, au dozi ya awali ya Tdap, hafai kupewa Tdap, isipokuwa sababu nyingine mbali na chanjo hiyo ipatikane. Bado wanaweza kupokea Td.
- Jadiliana na daktari wako ikiwa:
  - una kifafa au matatizo mengine ya mfumo wa neva,
  - umekuwa na maumivu au uvimbe baada ya chanjo yoyote yenye dondakoo, pepopunda au kifaduro, -
  ushawahi kuwa na ugonjwa unaoitwa Guillain-Barré Syndrome (GBS),
  - huhisi vizuri siku ya sindano ya chanjo.

## 4 Hatari

Unapotuma dawa zingine, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa sio makali na hupotea yenyewe. Mizio hatari pia inawezekana lakini ni nadra.

Watu wengi wanaopata chanjo ya Tdap huwa hawapati matatizo yoyote nayo.



U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

**Matatizo yasiyo hatari** baada ya kutumia Tdap
*(Hayakuathiri uwezo wango kufanya shughuli za kawaida)*

- Maumivu katika sehemu ya sindano (takriban vijana 3 kati 4 au watu 2 wazima kati ya 3)
- Wekundu au uvimbe katika sehemu ya sindano (takriban mtu 1 kati ya 5)
- Homa kidogo ya angalau 100.4°F (hadi takriban kijana 1 kati ya 25 au mtu 1 mzima katika ya 100)
- Maumivu ya kichwa (takriban watu 3 au 4 kati ya 10)
- Uchovu (takriban mtu 1 kati ya 3 au 4)
- Kichefuchefu, kutapika, kuharisha, maumivu ya tumbo (hadi kijana 1 kati ya 4 au mtu 1 mzima katika ya 10)
- Baridi, maumivu ya viungo (takriban mtu 1 kati ya 10)
- Maumivu ya mwili (takriban mtu 1 kati ya 3 au 4)
- Ukurutu, tezi zilizovimba (sio jambo la kawaida)

**Matatizo wastani** baada ya kutumia Tdap
*(Yaliathiri uwezo wa kufanya shughuli za kawaida, lakini hayakuhitaji matibabu)*

- Maumivu katika sehemu ya sindano (hadi mtu 1 kati ya 5 au 6)
- Wekundu au uvimbe katika sehemu ya sindano (hadi takriban kijana 1 kati 16 au mtu 1 mzima kati ya 12)
- Homa zaidi ya 102°F (takriban kijana 1 kati ya 100 au mtu 1 mzima katika ya 250)
- Maumivu ya kichwa (takriban kijana 1 kati ya 7 au mtu 1 mzima katika ya 10)
- Kichefuchefu, kutapika, kuharisha, maumivu ya tumbo (hadi mtu 1 au 3 kati ya 100)
- Kuvimba mkono mzima uliodungwa sindano (hadi takriban mtu 1 kati 500).

**Matatizo hatari** baada ya kutumia Tdap
*(Sikuweza kufanya shughuli za kawaida; nilihitaji matibabu)*

- Uvimbe, maumivu makali, uvujaji damu na wekundu katika mkono uliodungwa sindano (nadra).

**Matatizo yanayoweza kutokea baada ya chanjo yoyote:**

- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matibabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takriban dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai, na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Mwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona au kelele katika masikio.
- Watu wengine hupata maumivu makali mabegani na huwa na ugumu wa kusongeza mkono uliodungwa sindano. Jambo hili hufanyika mara chache sana.
- Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio mkali. Mizio kama hii inayosababishwa na chanjo huwa nadra sana, inakadiriwa chini ya dozi 1 kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Kama tu dawa zozote, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha hatari au kifo.

Usalama wa chanjo hutajwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea: **www.cdc.gov/vaccinesafety/**

## 5 Na kukiwa na tatizo hatari?

**Ninafaa kutafuta nini?**

- Tafuta kitu chochote kinachokutia wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.
- Dalili za mzio mkali zinaweza kujumuisha mabaka ngozini, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, kasi ya mapigo ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu. Dalili hizi huanza baada ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

**Ninafaa kufanya nini?**

- Ikiwa unafikiria ni mzio mkali au jambo lingine la dharura ambalo haliwezi kusubiri, piga simu kwa 9-1-1 au umpeleke mtu huyo katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, mpigie daktari wako simu.
- Baadaye, mzio unafaa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (VAERS). Daktari wako anaweza kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov**, au kwa kupiga simu kwa **1-800-822-7967**.

*VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.*

## 6 Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa

Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoundwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiwa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na namna ya kuripoti madai kwa kupiga simu kwa **1-800-338-2382** au kutembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation**. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia.

## 7 Ninaweza kupata maelezo zaidi aje?

- Muulize daktari wako. Anaweza kukupatia kipeperushi cha furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
  - Piga simu kwa **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/vaccines**

Vaccine Information Statement
Tdap Vaccine - Kiswahili

2/24/2015

42 U.S.C. § 300aa-26

Office Use Only

Translation provided by Minnesota Department of Health